# Uchanganuzi wa Utafiti: Kupanga Familia Miongoni mwa Wakimbizi Walioko kwa Makazi ya Wakimbizi ya Nakivale, Uganda

Uchunguzi Uliofanywa na UNHCR, Tume ya Wanawake ya Wakimbizi na CDC

Juni – Agosti 2011

*RIPOTI YA WAHISANI WA JUMUIA*

## SISI NI NANI?

United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR) inaongoza na kuratibu kitendo cha kimataifa ili kulinda wakimbizi na haki zao ulimwenguni.

Tume ya Wakimbizi ya Wanawake ni shirika la kutetea lililoko New York, Marekani (Marekani). Inatetea mabadiliko katika sheria, sera na vipindi ili kuboresha maisha na kulinda haki za wakimbizi na wanawake wakimbizi wa ndani kwa ndani, watoto na vijana.

Vituo vya Udhibiti wa Ugonjwa na Kukinga (CDC) ni wakala ya serikali ya Marekani. CDC ina Kitengo cha Afya ya Uzazi na inaangazia afya ya uzazi ya wakimbizi na watu wakimbizi wa ndani kwa ndani katika mipangilio ya dharura na baada-dharura.

### KUPANGA UZAZI NA WAKIMBIZI

Kupanga uzazi ni uwezo wa watu na mume/mke kutarajia na kuwa na tamanio la kuwa na idadi ya watoto wanaotaka. Pia ni uwezo wao wa kuchagua nafasi kati ya watoto wao kupitia matumizi ya mbinu za kuzuia mimba. Chini ya sheria ya kimataifa ya haki za binadamu, ufikivu wa kupanga uzazi ya familia ni haki ya binadamu. Mkutano wa Uondoaji wa Mbuni Zote za Unyanyasaji Dhidi ya Wanawake (CEDAW) inasema kuwa watu wote na mume/mkewe wana "haki ya kuchagua idadi, nafasi na wakati wa kupata watoto." Kipindi cha Matendo kutoka kwa Mkutano wa Kimataifa wa mwaka 1994 kuhusu Idadi ya watu na Ustawi pia inafahamu haki ya mume/mke na watu "kuamua kwa hiari na kwa dhima idadi, nafasi na wakati wa watoto wao na kuwa na taarifa na njia za kufanya hivyo."

## KWA NINI TULIKUJA NAKIVALE?

Tulizuru Uganda ili kuchunguza kiwango ambacho wakimbizi wanatumia huduma za familia za kupanga uzazi katika Makazi ya Wakimbizi ya Nakivale, mahali ambapo wakimbizi Wakongo, Wasomali, Warwanda, Waburundi, Wahabeshi na Waeritria wanapoishi. Tulitaka kujifunza kuhusu kile watu wanachofikiria kuhusu upangaji uzazi na kama wanaweza kupata madawa ya kupanga uzazi; ni watu wangapi wanazozitumia, na ni huduma gani za kupanga uzazi wanazozipata katika vituo vya afya.



*Wanawake katika jumuia wamekusanyika katika mfjadala wa kikundi.*

## TULIFANYA NINI WAKATI WA ZIARA YETU?

Mwanachama moja wa Tume ya Wanawake ya Wakimbizi alizuru Nakivale kwa wiki saba kati ya Juni na Julai 2011. Yeye na timu yake ya wanachama 6 waliwahoji wanawake 540 wenye miaka ya uwezo wa kuzaa (miaka 15-49). Pia walikutana na wanaume 48, wanawake, na wasichana na wavulana waliobalehe katika majadiliano ya kundi, na kuwahoji viongozi wakimbizi wa jumuia ili kujifunza kuhusu mawazo yao kuhusu upangaji uzazi. Pia walizuru vituo

vinne vya afya na wakawahoji wafanyikazi wa matunzo kuhusu huduma wanazotoa. Kwa kuwasikiliza watu wa Nakivale, tulijifunza moja kwa moja kuhusu mawazo na tajriba yao. Tunashukuru kukutana nao na ruhusa yao kutuwezesha kugawa taarifa na hadithi katika njia inayofaa.

## NI NINI TULIJIFUNZA WAKATI WA ZIARA YETU?

Tulijifunza kwamba asilimia 16.1 ya wanawake wenye umri wa uwezo wa kuzaa kwa sasa wanatumia mbinu ya uzuiaji mimba. Ingawaje idadi hii ni kidogo, ni kubwa kuliko vile ilivyokuwa katika makazi. Mbinu za kawaida zinazotumiwa za upangaji uzazi ni sindano za wanawake ambazo zinadumu kwa miezi mitatu, tembe za kumeza za kuzuia mimba, tembe ambazo wanawake humeza kila siku, na mipira ya wanaume, mbinu inayotumiwa na wanaume. Mbinu za muda mfupi, pamoja na mipira, tembe na sindano, sasa zinatolewa na vifaa vya afya katika makazi.

Pia tulijifunza kwamba utamaduni na dini zinachangia jukumu muhimu katika mawazo ya wakimbizi kuhusu upangaji uzazi. Dhana ya kawaida katika makazi ni kwamba familia kubwa ni bora sana na ni vizuri kuwa na watoto wengi kwa sababu wengi wao walifariki wakati wa mapigano. Pia tulijifunza kwamba kuna taarifa isiyo sahihi inayogawa miongoni mwa wanachama wa jumuia kuhusu athari za dawa za kuzuia mimba, kwa mfano kwamba zinasababisha saratani na kufanya mtu asiweze kuzaa .


Ingawaje kuna kliniki za afya ambazo zina huduma za kupanga uzazi katika Nakivale, wakimbizi wanasema kwamba watu wengi wanahitaji kutembea masafa marefu ili wapate kliniki hizo, na kwamba huduma za kupanga uzazi mara nyingi huwa hazipewi kipaumbele. Baadhi ya watu walisema haja ya kuwa na huduma za vijana-kirafiki kwa sababu huduma za kupanga uzazi zinatolewa kwa wadi ya hospitali ya uzazi, ambayo ni mahali ambapo vijana waliobalehe hawataki kuonekana huko. Wengine walisema kwamba kitoaji mipira katika vituo vya vijana na maeneo mbali na vituo vya afya mara nyingi huwa tupu.

## NI NINI TUTAFANYA SASA?

Tume ya Wanawake Wakimbizi na UNHCR itagawa matokeo haya na mapendekezo ili kuboresha huduma za kupanga uzazi ya wakimbizi. Baadhi ya mapendekezo ni:

- Kuunda mbinu za muda mfupi za kupanga uzazi, pamoja na mipira na mbinu za muda mrefu, kama vifaa vya vipandikiza na vitanzi, vipatikane kwa wingi.
- Kuunda mfumo wa marejeo ili kuhakikisha kwamba wanawake wanajifunza kuhusu huduma za kupanga uzazi wakati wako kwa kliniki ya afya kwa sababu nyinginezo, na kwamba wanafuatiliwa vilivyo ili kuhakikisha wanapokea taarifa na huduma kama wanazitaka.
- Kuwasaidia wafanyikazi wa afya wa jumuia na watumishi wa vifaa vya afya zaidi na jumuia ili kuongeza utambuzi wa kupanga uzazi ya familia kupitia elimu.

## NI NINI UNAWEZA KUFANYA KAMA UNATAKA KUJIFUNZA ZAIDI KUHUSU KAZI YETU?




Ili kujifunza zaidi kuhusu upangaji uzazi ya familia katika Nakivale, nenda kwa Kambi ya Kituo-Afya cha GIZ. Unaweza pia kutembelea Kituo Msingi cha Afya cha GIZ-Kiretwa, Medical Teams International (MTI) Kituo cha Afya-Juru, au Africa Humanitarian Action (AHA) Kituo cha Afya-Juru. Au wasiliana na Dkt. Stephen Mwaura, Mratibu wa Afya na Lishe katika UNHCR kwa nambari 0772-701049.

Kujifunza mengi kuhusu Tume ya Wanawake ya Wakimbizi ya uteteaji kwa niaba ya wanawake waliolazimishwa kuhama, watoto na vijana, tembelea www.womensrefugeecommission.org au wasiliana nasi katika mailto:info@wrcommission.org.

Picha: Tume ya Wanawake ya Wakimbizi/Neha Mankani.

Ripoti hii iliandikwa na Erin McCoy.

Women's Refugee Commission | 122 East 42nd Street | New York, NY 10168-1289
212.551.3115 | info@wrcommission.org | womensrefugeecommission.org

Nov. 2011